OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

SHULE YA SEKONDARI KICHANGA

S. L. P 43002, DAR ES SALAAM

SIMU 0713815185/0784815185

EMAIL:kichangasecondaryschool@gmail.com

KUMB. NA.
JINA LA MWANAFUNZI……
S. L. P……
DAR ES SALAAM.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KICHANGA WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2021.

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza (1) katika shule hii kwa mwaka 2021.

Shule ya Sekondari Kichanga ipo umbali wa Kilomita 2 kutoka Tandika Sokoni na Kilomita 2 kutoka Mtongani.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 hivyo mwanafunzi wa kidato cha kwanza anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/01/2021.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

a) Kufika shuleni ndani ya siku zilizopangwa
b) Kuhudhuria Orientation course inayochukua wiki sita toka siku ya kufungua shule
c) Njoo na picha (passport size) za hivi karibuni za mwanafunzi Pamoja na mzazi/mlezi

2.1. SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule hii ni SURUALI (KIJIVU) 2 (**isiwe modo**) na SHATI NYEUPE 2 kwa Wavulana na SKETI ZA KIJIVU 2 na SHATI NYEUPE 2 kwa Wasichana.
b) Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule (Kitambaa cheupe cha kichwani na shati au nusu kanzu nyeupe) na sketi ndefu ya rangi ya KIJIVU.
c) Viatu vyeusi vya kamba na soksi nyeusi kwa Wavulana na nyeupe kwa Wasichana.
d) Sare ya Michezo kwa shule hii ni T-shirts za kijivu kwa Wavulana na Wasichana.

2.2. VIFAA VYA DARASDANI

a) Daftari (Kaunta) 12
b) Mathematica set (mkebe kwa ajili ya somo la hesabu) 1
c) Kalamu za wino na risasi (pencil)
d) Daftari ndogo za mazoezi 12 (Home work)
e) Awe na karatasi za kutosha za kufanyia mitihani ya asubuhi (Rimu)

3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya Mwaka 1995. Aidha, tunazingatia miongozo yote inayotolewa na **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi** yenye dhamana ya kusimamia elimu nchini na **Ofisi ya Rais - TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni muhimu.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine halali utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa Sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za Umma.
j) Uwe na nywele fupi bila kunyoa kipara, ndevu au masharubu zinyolewe kwa wembe. Wasichana hawaruhusiwi KABISA kusuka nywele.
k) Hairuhusiwi kufuga kucha, kupaka rangi, hina, wanja na urembo mwingine kama vile kutinda nyusi, kuvaa hereni, pete, culture, kupaka piko pia hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na vya Jeshi.
l) Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda isiyoendana na mavazi rasmi ya shule. Mkanda unaoruhusiwa ni wa rangi nyeusi na wa ngozi.
m) Hairuhusiwi kumiliki silaha ya moto au kifaa chochote chenye ncha kali kwa mfano wembe, kisu na bisibisi.

3.1. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, kubeli na mengine ambayo ni haramu kisheria.
e) Kumpiga mwanafunzi mwenzako, mfanyakazi au mtu wa familia ya mfanyakazi.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa na nembo nyingine za Taifa.
h) Kuoa au kuolewa
i) Kupata mimba, Kutoa mimba
j) Kugoma kuchochea au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kuwa na simu ya mkononi
m) Kumnyanyasa mwanafunzi kwa sababu ya ugeni wake au jinsia yake au umbile lake au dini yake au rangi ya ngozi yake.
n) Kumtukana matusi mwalimu/mfanyakazi au mwanafunzi mwenzako au kutoa lugha yoyote ya maudhi/kufedhehesha.

3.2. **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi wakati wa kuripoti.**

a) Medical Examination Form ambayo inatakiwa ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule ikiwa imefungwa ndani ya bahasha.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Utawala wa shule.

MUHIMU: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia kila la kheri katika maandalizi ya kujiunga na shula ya Sekondari Kichanga.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KICHANGA

.....

MBWANA H. MBWANA

KIAMBATISHO I

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SECONDARI KICHANGA

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi. .....
2. Tarehe ya kuzaliwa.....
3. Utaifa.....
4. Uraia.....
5. Dini.....
6. Shule alizosoma kabla ya kuja Shule ya Sekondari KICHANGA

SHULE YA MSINGI	TAREHE NA MWAKA ALIOMALIZA	TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA

SAHIHI YA MWANAFUNZI ..... TAREHE.....

B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI

1. Jina kamili la mzazi .....
2. Utaifa .....
3. Uraia .....
4. Anuani ya mzazi .....
5. Sehemu anayoishi .....
6. Mtaa .....
7. Namba ya nyumba .....
8. Namba ya simu:- Nyumbani .....
   Ofisini .....

C. MAELEZO YA KIKAZI

1. Kazi ya mzazi .....
2. Jina la mwajiri .....
3. Anuani .....

Sahihi ya mzazi/mlezi ..... Tarehe .....

D. TAARIFA YA MAKAZI YA MWANAFUNZI

1. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi wanaishi
   Mtaa .....
   Kata .....
   Wilaya .....
2. Jina la mjumbe ..... Saini .....
   Muhuri ..... Namba ya simu .....
3. Jina la mwenyekiti/mtendaji wa mtaa ..... Saini .....
   Muhuri ..... Namba ya simu .....

E. UTHIBITISHO WA TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI.
(Uthibitisho huu utatolewa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi aliyomalizia Darasa la saba)

.....

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI YA UTII

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KICHANGA
S. L. P 43002
DAR ES SALAAM

I. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi.....(Jina kamili)
Ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga Kidato cha ……mwaka …… katika Shule ya Sekondari Kichanga.

NINAAHIDI KWAMBA:

1. Nitatii sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyosoma.
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi pamoja na shughuli zote za shule kwa kushirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli zote za kitaaluma.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali iliyopita bora bila kuitia hasara shule kwa uharibifu au kupoteza malighafi (raw materials) ya uzalishaji mali.
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari KICHANGA.

MUNGU NISAIDIE

Saini ya mwanafunzi..... Tarehe …….

II. KWA MZAZI/MLEZI

Mimi.....(Jina kamili) mzazi/mlezi wa mwanafunzi …….

NINAAHIDI KWAMBA:

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote nitakapohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu.
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (Home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Ninaahidi kulipa fidia ya gharama za uharibifu zitakazosababishwa kwa uzembe au makusudi na mwanangu pindi awapo shuleni.

MUNGU NISAIDIE

Saini ya Mzazi/mlezi..... Tarehe ……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION: KICHANGA SECONDARY SCHOOL

DATE: .....

PART A:

TO
Medical Officer
.....
.....

Miss/Mr.....
Please examine the above named as to her/his fitness for admission as a student in the following common disease/problem.

- ✓ Put a tick for Positive and a cross X for Negative in a box provided.

Test	Result
Pregnancy	
Asthma	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
TB (Tuberculosis)	
Sickle Cell	
Heart Disease	
Yellow fever	
U. T. I	
Malaria	

PART B: MEDICAL CERTIFICATION
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named and consider that she/he is physically FIT/UNFIT for admission above.

Date..... Signature.....

Station..... Designation.....